



MUHARRAM 1448 HIJIRIA - JULAI 2026 MILADIA (Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

SI NCHI ZILIZOKUWA ZA KIKOMUNISTI WALA ZA KIBEPARI ZA MAGHARIBI ZITAIOKOA TANZANIA



Jumatano tarehe 3 Juni, 2026, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya ziara ya kiserikali ya siku tatu nchini Urusi. Ziara hiyo ilijumuisha mkutano wake na Rais Vladimir Putin, kutoa hotuba katika Kongamano la 29 la Kimataifa la Jukwaa la Uchumi la St. Petersburg na pia alitunukiwa shahada ya udaktari na Chuo Kikuu cha Urafiki cha Urusi (RUDN University).

Hii ilikuwa ni ziara ya kwanza tangu mwaka 1969 kwa Rais wa Tanzania kutembelea Urusi. Raisi Samia alikuwa na mazungumzo ya kina baina ya nchi hizo mbili na mwenzake wa Kremlin Rais Vladimir Putin kuhusu kutanua ushirikiano katika biashara, nishati, kilimo, elimu, utalii, pamoja na mikataba ya madini, ukiwemo mradi wa urani wa Mto Mkuju wenye thamani ya dola bilioni 1.2. Kwa mujibu wa serikali ya

Moscow, biashara baina ya nchi hizi mbili (Tanzania na Urusi) imeongezeka kwa asilimia 25 mwaka jana. Uzania wa biashara kati ya Tanzania na Urusi ni karibu dola milioni 307 (€264 milioni) kwa mwaka, lakini kutokana na Baraza jipya la Biashara kati ya Russia na Tanzania lililoundwa Januari mwaka huu, takwimu hiyo inatarajiwa kuongezeka. Kwa mujibu wa takwimu za UN Comtrade za mwaka 2024, Tanzania iliagiza bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 295 kutoka Urusi na kusafirisha bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 9 pekee nchini Urusi. Kwa hiyo, kama walivyo mabepari wengine wa Magharibi, Urusi inainyonya Tanzania kwa jina la biashara huria, utandawazi na uwekezaji kutoka nje.

Tanzania ina rundo la rasilimali katika madini, ardhi kubwa ya kilimo, na maziwa makubwa, pia ina ufukwe mrefu wa Bahari ya Hindi ambayo ni nyeti kwa

Inaendelea Uk. 3

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

[قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ
وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ]

**“Imekwisha fichuka
chuki yao katika mido-
mo yao. Na yanayo
ficha vifua vyao ni ma-
kubwa zaidi.”**

[Aal-i-Imran: 118]

Kansela wa Ujerumani Friedrich Merz alitangaza mnamo Ijumaa kupinga kwake Muungano wa Ulaya kuweka vikwazo kwa umbile la Kiyahudi, huku Ufaransa ikitangaza kwamba haitakubali kuondoa vikwazo vilivyowekwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Iran isipokuwa makubaliano yoyote ya mwisho kuhusu mpango wake wa nyuklia yajumuishe kushughulikia mpango wake wa makombora ya masafa marefu na uungaji mkono wake kwa makundi yenye silaha katika eneo hilo.

Viongozi wa Magharibi wanaendelea kufichua uovu wao na chuki yao ya ndani. Huku wakishuhudia uhalifu wa kikatili unaofanywa na Mayahudi dhidi ya Waislamu Waislamu nchini Palestina, Lebanon, na Iran, na kuona kiburi na ufisadi wao Duniani, wakipuza maadili, kanuni, na

Inaendelea Uk. 3

Yaliyomo :

- ♦ Hijra ni ujumbe wa kimapinduzi sio kuongezeka miaka tu.....2
- ♦ Mikataba miwili katika mkataba mmoja.....4
- ♦ Miamala ya bima kikaangoni 5
- ♦ Makubaliano ya Irani na Marekani.....7

HIJRA NI UJUMBE WA KIMAPINDUZI SIO KUONGEZEKA MIAKA TU

Mwaka mpya wa Kiislamu unafungamanishwa na tukio kubwa na tukufu la Hijra. Hijra ya Mtume (SAAW) isitukumbushe kuongezeka miaka tu na kugeuka muda, kwamba jana tulikuwa mwezi wa Dhulhijja 1447 na leo tumeingia mwezi wa Muharram 1448 ndani ya mwaka mpya. Bali litukumbushe kwamba tukio ndilo lilobadili ulimwengu ukanyenyekea chini ya uongozi wa Uislamu chini ya Mtume SAAW kwa kufuata mwongozo wa Muumba (SW).

Mtume (SAAW) alipoingia Madina akapokewa kwa shangwe na hoihoi, kwa kuwa watu walikua na matarajio mapya na nidhamu mpya yenye matumaini ya kweli kwa viumbe.

Bila shaka maswahaba walikua na kila sababu ya kufurahia ujio wa Mtume SAAW ndani ya Madina, kwa kuwa wametoka katika kipindi kigumu cha kudunishwa na nidhamu ya kikafiri ya kijahilia, sasa wamegeuka kuwa wasimamizi wa mambo yote kwa msingi wa imani yao ya Uislamu. Hakuna tena anayethubutu kuwa kin-yume nao na kuwatambia. Muda wa kuwarudia waliokuwa wakiwadhulumu na kulipiza kisasi hapa hapa duniani uliwadia. Uislamu ukawa umedhihiri na ukafiri umedhalilika, na makafiri wakawa sio watukufu tena.

Siku ya Hijra ndio ambayo maswahaba pamoja na Mtume SAAW walifurahika, lakini walifurahikia nini? walifurahikia kushindwa kwa Abu Jahil,



Abu Lahab na makafiri wengine na ukafiri wao.

Hijra ilileta kwa Mtume SAAW na masahaba kupindua fikra mbovu za majahili kama akina Abu Jahil, Abdallah bin Ubayya bin Saluul (la.) nk. na kujikomboa kutokana na unyonge wa kuzuiliwa kutotekeleza wanachokiamini wakawa wanaungua nyoyo zao kwa kushinikizwa na kuzishuhudia kufu na munkraat/uovu mbele ya macho yao, huku wakizuiwa kuziondoa.

Leo Waislamu hali zetu tupo katika kukandamizwa na ukafiri, kudhulumiwa, kuteswa, kuuwawa na kuporwa rasilimali zetu na kuwaneemesha na kupambua miji ya makafiri. Hali hiyo imepelekea mpaka baadhi ya Waislamu kimakosa wameghururika ukawa huna cha kuwaambia, ukiwatajia nchi za mabepari na udhaifu wa mfumo wao hawavuki zaidi ya maendeleo ya mabepari ya kimaada tu, na kutupilia mbali masuala ya kiroho.

Na baadhi yao kimakosa hufurahia hali ya viongozi katika biladi za Waislamu namna walivyo katika kuvuruga utajiri wa Umma.

Kwa hivyo, kuzungumzia kuingia mwaka mpya bila ya malengo mapana na hatua za kujikomboa kutakuwa kama

mfungwa aliye gerezani akishereheka kuongezeka kipindi cha kifungo chake, huku gereza likizidisha udhibiti wake, ilhali nje ndio kumejaa kheri na salama yake.

Lazima Umma wa Kiislamu ukumbuke kuwa madola ya magharibi chini ya kinara Marekani wanaendelea kuuhujumu Uislamu na kuuwa Waumini wake. Hatuna sababu ya kufurahika kwa kuingia mwaka mpya, ikiwa hatufanyi jitihada za dhati kujiondoa katika idhilali zilizotuandama.

Lazima tumuitikie Mola wetu katika qadhia ya kusimamia ulimwengu huu kwa mfumo wa Uislamu na kuishi kwa Muongozo wake katika kila kipengee cha maisha yetu chini ya dola ya Kiislamu ya Khilafah Rashidah.

Mhariri

01 Muharram 1448 Hijria

Julai 2026 M

jukwalakhilafah@gmail.com

uchumi, kijiografia na njia nyeti ya kupitisha utajiri wa madini ya Kongo na bidhaa za nchi nyingine za nchi jirani zisizokuwa na bahari, lakini Tanzania imekosa msuli wa kimfumo. Kwa sababu hiyo, inakumbatia mataifa yaliyokuwa ya kikomunisti ya Urusi na China kwa ajili ya ulinzi kama njia ya kujihami na kuangalia uwezekano wa mbadala wa mbadalala wa unyonyaji wa Marekani na Ulaya.

Hata hivyo, matarajio ya Tanzania na mataifa mengine yanayoendelea kwa mataifa yaliyokuwa ya kikomunisti matmumanini hewa na yako mbali na ukweli. Kwa hakika, baada ya kifo cha kikawaida cha cha mfumo wa kikomunisti hususan kusambaratika kwa uliokuwa Muungano wa Kisovieti katika miaka ya 1990's, nchi zote mbili zilizokuwa za Kikomunisti za Urusi na China ziliishia kukumbatia mfumo wa kibepari na kuitekeleza ndani ya nchi zao.

Kwa hivyo, chini ya ubepari, suala la unyonyaji ndio lengo lao na haliepukiki. Hii ina maana kwamba mataifa yanayoendelea lazima yafahamu kwamba mataifa yaliyokuwa ya kikomunisti ya kijamaa na mataifa ya kibepari ya magharibi ni pande mbili za sarafu moja, zinafanana, na haziko mbali na ukoloni na unyonyaji.

Said Bitomwa

Mjumbe wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir in Tanzania

makubaliano yote—kuwaua wato-to, wanawake, na watu wasio na ulinzi, na kuharibu kila kitu kilicho njiani mwao—Chansela wa Ujerumani anatangaza kukataa kwake kuweka vikwazo kwa umbile la Kiyahudi, ingawa vikwazo hivyo vinaweza kuwa vya nembo tu na havina athari halisi uwanjani. Anakataa wazo hilo kabisa kwa sababu Waislamu na ardhi zao ndio waathiriwa. Vile vile, Ufaransa inakataa kuondoa vikwazo kwa Iran hadi itakaposaini ahadi na makubaliano yanayohakikisha kwamba Iran haitainuka tena na kutishia umbile la Kiyahudi.

Mandhari hii inaashiria chuki inayofurika kutoka pande zao kuelekea kila kitu kinachohusiana na Uislamu na Waislamu. Hawawezi kuvumilia kuweka chuki hii ndani ya nafsi zao, kwa hivyo inajitokeza kuwafichua na kufichua uadui wao wa waziwazi dhidi ya Uislamu na Waislamu na upendo na uaminifu wao kwa Mayahudi wanyakuzi, hata kama watafanya ukatili na mauaji ambayo hata wanyama wa pori wangejepusha nayo.

Huyu ndiye kafiri Magharibi, ambaye anadai kujali usalama, utulivu, amani, na haki za binadamu, lakini kiuhalisia, anatafuta kuwatawala Waislamu na ardhi zao. Anatamani usalama na amani, lakini si kwa Waislamu au wadamu wote; badala yake, anatafuta kwa wakoloni makafiri pekee. Anatamani utulivu na amani, lakini si kwa Waislamu au ardhi zao; badala yake, anatafuta amani inayodhamini maslahi yake na kuzifanya nchi zetu zimtii. Anatamani haki za binadamu, lakini si kwa watu wote; badala yake, anazitafuta kwa ajili ya makafiri

pekee, si kwa Waislamu. Hili ndilo umbile halisi la kafiri Magharibi, na yeyote anayefikiri vyenginevyo amedanganywa. Waislamu hawana nusra au msaidizi isipokuwa wao wenyewe, baada ya Mwenyezi Mungu (swt). Ni wana wao tu katika majeshi ndio watakaowakomboa wao na ardhi zao kutokana na udhalilifu na ukoloni. Hivyo basi, toeni msaada wenu (Nusra), Enyi majeshi!

إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ

“Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf- sini mwao.” [Ar-Ra’d: 11]

**Afisi Kuu ya Habari
ya Hizb ut Tahrir**



MIKATABA MIWILI KATIKA MKATABA MMOJA

Swali:

Kijana kutoka Tunisia anataka kununua gari kwa njia ya Halal. Kuna mtu akamuelekeza kwa kampuni fulani inayokodisha gari kwa muda mrefu ambayo pia kuna uwezekano wa kuimiliki baada ya kuisha kwa mkataba wa ukodisha. Ikimaanisha kuwa hii ni mikataba miwili. Je inaruhusiwa?

Jibu:

Mikataba katika Uislamu ni mepesi na iko wazi; na mkataba mmoja hauchanganywi na mkataba mwengine. Kinyume na hali ilivyo katika sheria za kibinadamu.

Mtume (saw) ameharamisha kufungwa kwa mikataba miwili kupitia mkataba mmoja: Mfano mtu kusema nakuuzia nyumba yangu kwa sharti ununue na nyumba yangu nyengine au nakuuzia nyumba yangu na wewe uniuzie nyumba yako. Hilo haliruhusiwi kwa kuwa ni mikataba miwili iliyojumuishwa katika mkataba mmoja, kwani ukisema **nakuuzia nyumba yangu** ni mkataba wa kwanza na ukisema **kwa sharti nami uniuzie nyumba yako** ni mkataba wa pili na yote imejumuishwa katika mkataba mmoja. Imesimuliwa kutoka kwa Ahmad Abdul Rahman bin Abdullah bin Masood, kutoka kwa babake, alisema:

“Mtume (saw) ameharamisha mikataba miwili ndani ya mkataba mmoja”

Hivyo kutokana na suali lako, kuna mkataba wa ukodishaji wa gari kwa muda fulani kisha baada ya muda huo unakuwa ni mkataba wa uuzaji wa gari. Makubaliano



hayo mawili ya ukodishaji na uuzaji wa gari kati ya mmiliki wa gari na mkodishaji wa gari yako ndani ya mkataba mmoja. Hivyo kwa mujibu wa Hadith hiyo hairuhusiwi.

Ama ungetaka suluhisho, ungelikubaliana na mwenye gari akuuzie gari hilo kwa mkopo, umpe kima cha kuanzia na kima kitakachobakia ukamlipa kidogo kidogo mpaka utakapokamilisha bei muliokubaliana hapo awali, na kwa hali hiyo gari hilo litakuwa ni lako kwa mujibu wa mkataba wa mauziano muliokubaliana awali. Mkataba huu ni mkataba wa mauziano kwa mkopo na unaruhusiwa **lakini kwa sharti ya kuwa bei ya uuzaji iwekwe wazi tangu mwanzo wa mkataba ima ni kwa malipo ya mkono kwa mkono au ni malipo ya mkopo wa kulipa kidogo kidogo, na mkataba wa mauziano hufungwa kwa makubaliano ya wahusika.**

Kwa hivyo ikiwa wote wamekubaliana juu ya bei fulani, na muuzaji akamuuzia mnununuzi kwa bei ya mkono kwa mkono (cash) na mnunuzi akakubali au akamuuzia kwa bei ya mkopo na mnunuzi akakubali, hili **linaruhusiwa** maanake ni kujadiliana juu ya bei ya uuzaji sio uuzaji. Kujadiliana kumeruhusiwa. Imesimuliwa na Anas bin Malik kuwa Mtume (saw) aliuza blanketi na bakuli la kunywa maji akasema: *“Nani atakaye nunua*

blanketi na bakuli la kunywa maji?” Bwana mmoja akasema: *Nitazinunua kwa Dirham moja. Mtume (saw) akasema: “Nani atakayetoa zaidi ya Dirham? Nani atakayetoa zaidi ya Dirham? Bwana mmoja akakubali kumpa Dirham mbili, Mtume (saw) akamuuzia.*

Vilevile, wengi wa wanavyuoni wamesema ya kwamba inaruhusiwa kuuza kitu kwa mkopo kwa bei ya juu kuliko bei yake ya mkono kwa mkono (cash). Imesimuliwa ya kwamba Tawoos, Al-Hakam na Hammad walisema kuwa hakuna makosa ikisemwa: **Nakuuzia kwa bei kadhaa ikiwa ni mkono kwa mkono na kwa bei kadhaa ikiwa ni kwa mkopo, naye atachagua moja kati yao.** Imam Ali (ra) alisema: **Yoyote mwenye kuuza kwa bei mbili; moja ya mkono kwa mkono na nyengine ya mkopo, basi na ataje mojawapo kabla ya kufunga mkataba.**

Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.

Ndugu yenu

Atta Ibn Khalil Abu Al-Rashtah

Miamala ya bima iwe iwayo ni miamala haramu isiyo na shaka, licha ya baadhi ya Waislamu na taasisi kuibeba na kuonesha ni halali. Bima haisihi kwa sababu nne kubwa:

Kwanza, kusema shirika la bima ni dhamana juu ya bidhaa, mali, nyumba au maisha sio sahihi. Kwani shirika la bima hata kama likijiita la Kiislamu kamwe halidhamini vitu hivi, bali inachokifanya ni kufunga mkataba wa kumlipa mteja fedha taslimu au kumlipa mbadala wa kitu kama kilichoharibika, na wakati mwingi baada ya kumsumbua na kumzunguusha. Lakini kamwe shirika halifanyi kazi ya kukilinda (kuchukuwa dhamana) kivitendo kitu husika au kulinda maisha ya mtu, bali inachokifanya shirika la bima ni kuingia mkataba wa kulipa pesa baada ya gari lako kuharibika, nyumba yako kuungua moto au kufa kwa mtu, lakini si dhamana ya kitu.

Pili, Kiislamu ili mkataba wowote usihi lazima utimize masharti maalum. Mbali na kupatikana ijabu (offer) na qabuli (acceptance), pia mkataba wa Kiislamu lazima ufungwe juu ya kupatikana manufaa/manfaa (ainu). Na lau kama mkataba haukufungwa juu ya kupatikana manufaa/ manfuu au 'kitu maalum', Kiislamu mkataba huo huwa batili. Na manufaa katika mkataba hudhihirika katika sura zifuatazo: Kwanza, amma ufungwe juu ya kitu kwa mbadala wa kitu.

Kama kuuza na kununua. Pili, au ufungwe juu ya kupatikana kitu/manufaa bila ya mbadala. Kama kutoa tunu/zawadi. Tatu, au uwe mkataba juu ya manufaa kwa badala. Kama ajira. Na nne, au uwe mkataba juu ya manufaa bila badala. Kama kuazima kitu nk. Yaani lazima mkataba wa kiislamu ufungwe juu ya kupatikana kitu au manufaa fulani. Lakini mkataba wa bima haukufungika katika hali hii, bali ni makubaliano tu ya mteja kulipa kiwango fulani cha fedha kwa shirika la bima. Amma mteja wa bima kuja kulipwa fedha, au kufidiwa mali yake na shirika la bima kufuatia kupata ajali gari yake, kuungua nyumba, kupata ulemavu, kufa, nk. kamwe malipo hayo hayazingatiwi kisheria kuwa ni sehemu ya manufaa yenye uhusiano na mkataba wa mteja kulilipa shirika la bima. Bali kisheria ni mkataba mwengine kando kama tutakavyofafanua katika hoja yetu ya tatu inshaAllah.

Tatu, Kiislamu mkataba haufungwi katika hali ya mazingira yenye utata na yasio na uhakika kujiri kwake. Ikiwa kuna hali fulani isiyo na uhakika kutokea kwake haifai kufungwa mkataba kwa mkabala wa hali hiyo. Bali Kiislamu lazima mkataba ufungwe kuwafikiana na hali iliyopo au yenye uhakika kujiri kwake. Kwa hivyo, shirika kusema kwamba litakufidia gari yako 'endapo ikipata ajali' au litaku-jengea nyumba mpya 'endapo ikiungua moto' au litaku-gharamikia matibabu 'endapo ukiumwa' nk. Hizo zote ni hali za utata zisizokuwa na uhakika kutokea kwake. Uislamu ni dini tukufu yenye murua, insafu na uadilifu, kamwe haiwezi

kuhalalisha mkataba wa aina hii wa kitapeli unaopelekea dhulma ya wazi. Kwa hivyo, mkataba wa aina hii huwa si mkataba Kiislamu, kwa kuwa unamfunga mtu na mkabala wa hali isiyokuwa na uhakika kujiri au kutojiri kwake.

Nne, kwa mujibu wa Uislamu istilahi ya dhamana hukamilika kwa kupatikana masharti mata-tu ya lazima: Kwanza, apatikane anayekubali kubeba mzigo wa dhamana (dhwaminu). Pili, awepo anayesaidiwa kwa kuchukuliwa dhamana (madhumuun anhu) Na tatu, pia awepo mwenye kudai (madhwmuunu lahu)

Ama mdhamini, yeye lazima akubali kuchukuwa na kujitwisha dhamana pasina kupata malipo yoyote kwa udhamini wake huo. Kwa mujibu wa sheria za kiislamu, mdhamini aki-hitaji malipo kwa udhamini, basi huwa amekosa sifa ya kuwa mdhamini. Amma anayesaidiwa kuchukuliwa dhamana kulipa, nae asilipe malipo aina yoyote kwa dhama-na hiyo. Na hilo deni linalochukuliwa dhamana lazima iwe ni haki ya mali ya wajibu, yaani iwe ni lazima kulipwa si khiyari. Na lau kama ni haki ya mali ambayo si wajibu kulipwa, hapo huwa hakuna dhamana. Ukiangalia katika mashirika ya bima hayajatimiza masharti haya, bali yamekhalifu wazi wazi kabisa. Kwani anaekata bima (shirika, sacco, NGO au mtu binafsi) hafanyi bure bali

Inaendelea uk 6

kwa malipo yanayoambatana na mashariti yenye vikwazo, kijanja janja na ya kitapeli. Ama kwa upande mwingine katika mkataba wa bima, hakueleweki juu ya watatu hawa yaani: mdhamini, mdhaminiwa na wala deni. Hadithi iliyopokelewa na Abu Daud kutoka kwa Jabir inatoa mwanga wa jambo hili:

Anasema: alikuwa Mtume SAAW hamswalii mtu aliyekufa na deni, basi siku moja akaletwa maiti, Mtume akauliza, 'je anadaiwa mtu huyu?' Wakasema ndio anadaiwa dinaari mbili, Mtume akasema 'basi mswalieni maiti wenu', Abu Qatada akasema nitazilipa mimi erwe Mtume wa Allah, basi Mtume akamswalia. Na zama Allah alipo mpa Mtume ushindi (katika vita kadhaa na dola ikawa na pesa) Mtume akasema: 'Mimi nina haki zaidi kwa muumini kuliko hata nafsi yake (yeye mwenyewe) basi atakayekufa na akaacha mali, mali hiyo watarithi warithi wake, na atakayeacha deni basi nitalilipa mimi'

Hadithi hii ipo wazi kwamba kumepatikana watu watatu: Mdai, mdaiwa na mdhamini wa deni. Abuu Qatadah alikuwa mdhamini na hakupata malipo kwa udhamini wake, maiti alikuwa mdhaminiwa na juu yake hapakuwa na deni tena wala malipo ya aina yoyote kwa kudhaminiwa huko, na pia alikuwepo mdai aliyekuwa akimdai maiti. Katika mkataba wa bima hakuna hali hii, kwani hakuna watu watatu hawa katika mkataba huu. Kwa hivyo, bima ni haramu hata kama ikipachikwa jina lolote lile, maadamu inafunga mkataba kwa mtindo huu wa kikafiri. Na kamwe Waislamu wasiangalie jina la mkataba, bali waangalie

waaqiya/uhalisia ya mikataba hiyo, jee inawafikiana na hukumu za kisheria au laa?

Hivyo, kushiriki kwa khiyari katika kitu kiitwacho bima ni *haramu mutlaq* na anayekula fedha za bima anakula moto. Aidha, ni batili kuasisi michakato yoyote hata ikiitwa 'bima ya Kiislamu' bali hatari na uharamu wake huongezeka zaidi pale itakapoitwa bima ya Kiislamu. Kwani huko ni kuuhalalisha ukafiri kwa kuuvisha kijanja guo la Kiislamu. Mtume SAAW anasema katika Hadithi aliyoipokea kutoka kwa Mola wake (hadithi- Qudsi).

'Hakika mtu mwenye adhabu kali siku ya Qiyama ni aliyetumia jina langu akajingizia kipato chake binafsi'.

Kwa ufafanuzi huu wa uharamu wa bima utaweza kumnasua mukhlis na mchamungu kuacha dhambi hii. Sasa limebakia swali moja. Vipi kuhusu bima zinazosimamiwa na serikali kwa lazima kupitia nguvu ya sheria (statutory)? Jibu, kwa atakayeshindwa kuiepuka, hatohesabiwa kuwa amefunga mkataba huo kwa khiyari yake, bali hili huingia katika mlango wa kutenzwa nguvu. Lakini mtu anayekwenda mwenyewe na akafunga mkataba wa bima nyenginezo kwa khiyari, kama bima ya maisha, afya nk. kwenye taasisi zilizozagaa mitaani hadi misikitini na makanisani, mtu huyu huwa anatenda haramu ya wazi kabisa na tunamnasihi aache mara moja.

Mwisho lazima tukumbushane kwamba leo tumezingirwa kila upande na mfumo muovu wa kikafiri wa kirasilmali/kidemokrasia, kiasi cha kutenza nguvu na sheria zao kwa kuwa mfumo wao ndio unaotawala dunia. Ni wajibu kujipinda katika jukumu letu la kuirejesha tena dola

ya Kiislamu ya Khilafah Rashidah inayopaswa kuanzia katika nchi kubwa za Waislamu ili ije kuwa kinga ya kudumu na kutuepusha na miamala mbali mbali ya haramu.

MATUKIO YA MUHARAM

1. Mwaka Mpya wa Kiislamu.

Kuanza Mwaka Mpya wa Kiislamu.

2. Kuangamizwa Fir-aun na Kuokolewa Nabii Mussa. (A.S)

Allah alimnusu Musa A.s kwa kumuokoa na kuangamizwa Firaun.

3. Kuangamizwa Abraha na Majeshi yake baada ya Kutaka Kuivunja Al-kaaba.

(Tarehe 17 Muharram siku kama 50 kabla ya kuzaliwa SAAW. Mwaka wa 571 AD)

4. Mkataba wa Dhulma na Uadui dhidi ya Banu Hashim.

Makuraishi waliweka mkataba wa kuwagomea Banu Hashim na Banu Al-Mutwalib kwa kukataa kumtosa Mtume Saaw ili wamuuwe. (Mwaka wa 7 wa Utume).

5. Kubatilika kwa Mkataba wa Dhulma

Kuvunjika kwa Mkataba wa uadui wa Makuraishi dhidi ya Banu Hashim na Banu Al-Mutwalib baada ya kukosa kuungwa mkono na baadhi ya makabila yenye nguvu. (Mwaka wa 10 baada ya Utume).

Mnamo tarehe 17/6/2026, Bloomberg ilichapisha rasimu ya hati ya makubaliano ya awali yenye vipengele 14 (MoU) kati ya Marekani na Iran. Maudhui yake yalikuwa sawa kabisa na yale yaliyoripotiwa na Shirika la Habari la Iran la Mehr linaloungwa mkono na serikali ya Iran.

Kisha kulifuatia kutiwa saini kwa hati hiyo ya makubaliano ghafla kati ya Rais wa Iran na raisi wa Marekani, Trump, katika Ikulu ya Versailles nchini Ufaransa. Trump alitaka kuwakumbusha Waislamu kuhusu Mkataba wa Versailles baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, ambao ulisababisha kuanguka kwa Khilafah (Ukhalifa), dola ya Waislamu, na kuvunja umoja wao. Ni kana kwamba, kwa kuchagua Ikulu ya Versailles, ambayo hapo awali ilibadili mkondo wa historia kwa kufutwa kwa Khilafah, Trump anajaribu kujitangaza kama kiongozi anayefanya historia kwa kufuata nyayo za waliomtangulia.

Hayo yalifanyika chini ya usimamizi wa mpatanishi kati ya pande hizo mbili, Waziri Mkuu wa Pakistan Shehbaz Sharif.

Waraka huo wa mawafikiano umekuja licha ya ukweli kwamba Marekani, pamoja na "mshirika wake Netanyahu", ilikuwa imeanzisha operesheni ya kijeshi ya kushtukiza mwishoni mwa Februari iliyo-pita, ikiwalenga viongozi wakuu wa kisiasa na kijeshi wa utawala huo, hasa Kiongozi. Na Vita hivyo vilipangwa kudumu kwa siku nne, lakini vilidumu kwa siku arobaini, vikishindwa



kufanikisha lengo lao la kuuangusha utawala wa sasa au kuwaweka viongozi mawakala ili kuigeuza Iran kutoka dola inayozunguka ushawishi wa Marekani kuwa dola wakala.

Baada ya miaka 47 ya Iran kuwa ndani ya mzunguko wa ushawishi wa Marekani Marekani ililenga kuifanya kuwa dola wakala (tegemezi), hasa ilipoanza kuisukuma itoke katika maeneo ambayo hapo awali ilikuwa imeruhusiwa kufanya shughuli zake, kama vile Syria, Iraq, Lebanon na Yemen.

Mashambulizi ya Marekani na kijidola cha mayahudi ndani ya Iran ilisababisha baadhi ya watu nchini Iran kuanza kufikiria kujinasua moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa kuwa katika mzunguuko wa Marekani. Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu (IRGC) lilikuwa na nafasi kubwa katika hilo, kama tulivyoeleza awali tarehe 3/6/2026. Tulisema:

"...kama ilivyotokea Venezuela wakati majeshi ya Marekani yalipomteka nyara rais wake, na makamu wa rais pamoja na wasaidizi wake wakajisalimisha kwa Marekani. Hata hivyo, hali hiyo haikutokea Iran baada ya kuuawa kwa Kiongozi wake Mkuu, Ali Khamenei

Walinzi wa Mapinduzi wa Iran walibaki imara kukabiliana na uchokozi huo na kuwashambulia maadui... wakitafuta kujitegemea dhidi ya Marekani, tofauti na mremgo wa kisiasa wa Iran ambao unatamani kushirikiana na Marekani.

Uimara, nguvu na ushawishi wa Walinzi wa Mapinduzi ulitokana na nafasi yao ya awali katika kumchagua Kiongozi Mkuu mpya, Mojtaba ambaye aliwaunga mkono na kuwategemea ili kudumisha utawala wake. Hakukubaliana na hati ya makubaliano ya awali wala amani na Marekani baada ya Marekani kumuua baba yake, aliyekuwa Kiongozi Mkuu wa awali, pamoja na idadi ya maafisa wengine.

Hali hii ilibadilika baada ya uongozi wa kisiasa nchini Iran (Rais, Spika wa Bunge na Waziri wa Mambo ya Nje) kufanikiwa kumshawishi Kiongozi Mkuu (Mojtaba) kwamba Hati ya Makubaliano ya Awali (MoU) ilikuwa kwa maslahi ya Iran.

Hata hivyo, kauli ya Mojtaba kuhusu mawafikiano hayo ni kana kwamba alikuwa akimwajibisha rais wa nchi yake pamoja na maafisa wengine kwa madhara yoyote ambayo Iran ingeweza kuyapata kutokana na makubaliano hayo.

Baada ya hapo, sauti ya Walinzi wa Mapinduzi ikawa haina namna ilinyamaza kwa utiifu kwa Kiongozi Mkuu.

Kuidhinishwa kwa hati hiyo ya makubaliano na utayari wa Iran kutia saini na Marekani inaashiria Iran kurejea katika hali yake ya awali kama dola iliyopo katika mzunguuko wa Marekani, tofauti na msimamo wa awali wa Walinzi wa Mapinduzi uliokuwa ukitetea kujikomboa kikamilifu!

Mremgo wa kisiasa kwa kiasi fulani ulipata nguvu zaidi, huku lengo lake kuu likiwa ni

kuirejesha Iran katika nafasi yake ya zamani chini ya ushawishi wa Marekani, kama Uturuki, badala ya kuifanya kuwa dola wakala kama Misri, Syria na nchi nyengine za eneo hilo.

Hata hivyo inaonesha ushawishi wa Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu (IRGC) haujatoweka kabisa kama ilivyodhihirika walipojibu mashambulizi ya Marekani dhidi ya pwani ya mashariki ya Iran: Hati ya Makubaliano imeweka wazi kuwa Iran imekubali usitishaji wa kudumu wa mapi-gano, kutopigana tena, na pia nchi hizo “zitatangaza kusitishwa mara moja na kwa kudumu kwa operesheni za kijeshi katika maeneo yote ya mapambano, pamoja na Lebanon.

Hii ina maana kwamba Iran imeacha msimamo wake wa kupambana na Marekani, ambayo iliishambulia, ikawaua viongozi wake waandamizi na kuharibu vituo vyake vya nyuklia pamoja na miundombinu yake muhimu.

Aidha, Iran inathibitisha tena kwamba haitanunua wala kuendeleza silaha za nyuklia na wamekubaliana kutatua suala la hatima ya akiba ya urani zilizorutubishwa kwa mujibu wa utaratibu utakaoafikiwa Hati hii imepata fursa Marekani ya kuingilia mambo ya ndani ya Iran, jambo ambalo ni janga na baya zaidi!

Makubaliano haya yamejaa matumizi ya maneno yenye utata yanayoweza kufasiriwa kuleta maslahi ya Iran, au maslahi ya Marekani.

Miongoni mwa masuala hayo ni kuondolewa kwa vikwazo na kufunguliwa kwa Mlango wa Bahari wa Hormuz, Marekani kuondoa majeshi yake kutoka maeneo ya karibu na Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ndani ya siku 30 ambapo hapo awali Iran ilikuwa ikidai Marekani iondoe majeshi yake kutoka eneo lote la Mashariki ya Kati, na pia iachilie dola bilioni 12 za fedha za Iran zilizokuwa zim-ezuiwa na Marekani nk.

Kisha hati inatamka makubaliano ya mwisho yatapitishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Trump ameshindwa kufanikisha malengo yake kwa njia ya kijeshi na ameshtushwa na upinzani wa Walinzi wa Mapinduzi dhidi yake. Uhalisia sasa unamweka Trump chini ya shinikizo baada ya kupoteza mengi katika vita alivyoanzisha. Hadhi yake imeshuka sana, na imani kwake imepungua duniani kote, hata ndani ya Marekani na miongoni mwa wanachama wa chama chake pamoja na wafuasi wake. Bila shaka, hali hii itaathiri uchaguzi wa katikati ya muhula wa Bunge mwezi Novemba na baadaye uchaguzi mkuu miaka miwili baadaye. Kufungwa kwa Mlango wa Bahari wa Hormuz na Iran pamoja na Marekani kuweka mzingiro wkatika njia hiyo ya maji— ambapo hupitia takriban thuluthi moja ya tano ya mafuta ya dunia na gesi asilia iliyoyeyushwa (LNG)— kulisababisha kusimama kwa

shughuli za usafiri wa baharini. Hali hiyo ilisababisha kupanda kwa kasi kwa bei za mafuta na gesi, na kwa kawaida ikafuatiwa na ongezeko la bei za vyakula. Hali hii huathiri moja kwa moja uchaguzi wa katikati ya muhula. Kwa hivyo, Trump aliona fursa katika mazungumzo na Hati ya Makubaliano ya kupata ushindi wa kisiasa kupitia mazungumzo, ushindi ambao alishindwa kuupata kwa vita.

Trump hakupaswa kupewa ambacho alishindwa kukipata vitani hasa kwa kuwa Iran ni nchi kubwa sio dhaifu yenye takribani kilomita za mraba milioni 1.6, jiografia yenye ardhi kubwa, watu karibu milioni 90, pamoja na umuhimu mkubwa wa kimkakati. Pia ina mafuta, gesi na maliasili nyingine, uwezo wa kujitosheleza kwa chakul, viwanda vya kijeshi na kiraia, na nguvu ya nyuklia kwa kiwango cha karibu asilimia 60 na kufikia takribani kilo 440, kiwango kikubwa sana ikilinganishwa na kikomo cha asilimia 3.67 kilichowekwa katika makubaliano ya mwaka 2015.

Iran ingeweza kuwa huru kikamilifu kando na ushawishi wa Marekani Lakini makubaliano hayo yameiokoa Marekani iliyokwama kwenye ndoana kwa miezi minne.

Umma unahitaji kurudi katika uhai na heshima yake baada ya fedheha hii. kwa kurejesha dola ya Kiislamu ya Khilafah Rashidah. Waislamu tuna wajibu wa kufanya kazi ya ulinganizi tukiwa na yakini kwamba hali hii chini ya tawala za mabavu haitadumu kwa muda mrefu, Khilafah itarejea tena kwa ahadi ya kweli ya Allah Taala.

Makala hii mukhtasari wa makala ya ya karibuni ya Hizb ut Tahrir yenye anuani: “Hali halisi ya sasa ya Iran kufuatia kurejea upya mashambulizi baina yake na Marekani”